



# MIAKA 59 YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

1964 - 2023

## SUZA inavyoenzi malengo ya Mapinduzi kwa vitendo

Jese Mikofu, Mwananchi Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ni chuo kikuu pekee cha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kina dhima kubwa ya kusaidia Serikali katika ustawi wa jamii kwa kuzalisha wataalamu bora kwa kila sekta kwa mujibu wa mahitaji ya nchi na kufanya tafti zenye kuibua suluhisho kwa matatizo mbalimbali ya jamii

SUZA ni chuo kikuu kilichoshenehi fani mbalimbali zikiwemo Afya, Kilimo, Sayansi Asili na Sayansi Jamii, Ualimu, Tehama, Utalii, Biashara, Lugha na Habari.

Fani zote hizi ni muhimu na zinachangia ukuaji wa Uchumi, kijamii na kisiasa na asilimia kubwa ya wahitimu hawa tunaowatoa wameajiriwa kwenye sekta binafsi na Serikali ndani na nje ya Zanzibar.

Kwa muktadha huu SUZA chini ya Uongozi wa Mkuu wake ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Ali Mwinyi, Baraza la Chuo, Menejimenti ya Chuo na wafanyakazi wote tunaendeleza kivitendo fikra za Mapinduzi Matukufu ya Mwaka 1964.



Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (katikakti walioketi) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watendaji wa wizara hiyo na SUZA mara baada ya uzinduzi wa mradi wa utafiti wa kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto kabla na baada ya kujifungua.

Katika kuendeleza fikra hizo leo tutazungumzia mradi wa utafiti wa kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto kabla na baada ya kujifungua unaoendeshwa na SUZA kwa kushirikiana na Liverpool School of Tropical Medicine na Global Fund.

SUZA kupitia Skuli ya Afya na Sayansi za Tiba kilifanya utafiti kuhusiana na huduma za afya ya mama kabla na baada ya kujifungua.

Skuli hii inazalisha wahitimu wa afya kama vile Watabibu, Wauguzi na Wakunga na pia Maafisa Tabibu na kada shirik-

ishi ambazo zinafundisha jinsi ya kutoa huduma bora kwa mama na mtoto kabla na baada ya kujifungua.

Takwimu zinaonesha kuwa vifo vya mama na watoto vimekuwa ni tatizo kubwa linalohitaji uangalizi wa karibu zaidi hasa katika nchi za dunia ya tatu.

Hivyo, katika kutekeleza mpango kazi wa Taifa wa sera ya Afya na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), chuo kimekua katika mstari wa mbele katika kusaidia kutatua tatizo hilo kwa kushiriki katika kufanya utafiti kuhusu tatizo

la mama wajawazito kukumbwa na changamoto kabla na baada ya kujifungua kwa kuwa ni eneo muhimu kulifanyia kazi.

Mradi huu ulijikita kwenye utafiti wa awali ambao uliibua changamoto kuu mbili; ukosefu wa baadhi ya vifaa vya kutolea huduma za mama kabla ya kujifungua, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua na uhitaji wa mafunzo kwa watoa huduma kwenye hospitali na zahanati zetu ambao wengi wao wanahitaji mafunzo kwa ajili ya kuongeza ufanisi.

Wanautekeleza ni SUZA na Liverpool School of Tropical Medicine (LSTM) ikishirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar katika vituo vyake kumi vilivyopendekezwa na kudhaminiwa na Global Fund.

Vituo vyenyewe ni sita kutoka Unguja ambavyo ni Mwembeladu, Magogoni, Mwera, Bumbwisudi, Kivunge na Makunduchi, na vinne kutoka Pemba ambavyo ni Chakechake, Mkoani, Wete na Micheweni.

Kwa upande wa SUZA mradi ulizinduliwa mwanzoni mwa mwaka 2022 na utamalizika mwisho wa mwaka 2023. Mradi huu mpaka utakapomalizika utagharimu kiasi cha Dola za kimarekani 242,771.

Walengwa wa mradi ni wafanyakazi wa vituo vya afya ambavyo vinatoa moja kwa moja huduma za mama na mtoto, kuanzia ujauzito hadi kujifungua kwa mama na pia mtoto anapozaliwa.

Lakini pia jamii ambayo inapokea huduma katika vituo vya afya tajwa hususan mama kabla na baada ya kujifungua. Sababu kubwa ya kuwalinga wao ni kwa kuwa ndiyo wanaohudumia kina mama na

kuwapa elimu yote kuhusiana na uzazi.

Aidha hii imekuja baada ya matokeo ya utafiti kuonesha kuwa watoa huduma hawa wanahitaji ujuzi zaidi kuedana na wakati wa sasa.

Wafanyakazi hawa wanahitaji taaluma ya matumizi ya vifaa vipya, kwa kuwa wengi wao bado wapo kwenye matumizi ya yale ya zamani. Pamoja na hayo wahudumu hawa walipaswa kupewa taaluma ya kujitathmini baada ya kutoa huduma.

Matarajio baada ya kukamilika kwa mradi huu ni kuhakikisha huduma bora kwa mama kabla na baada ya kujifungua inapatikana katika vituo vyote vya afya hususan kwa kumuepusha mama na mtoto magonjwa ya kuambukiza kama vile Kifua Kikuu (TB), Malaria, Virusi vya Ukimwi na Ukimwi (HIV/AIDS).

Huu ni mwendelezo wa SUZA katika kuhakikisha inatimiza malengo ya Mapinduzi Matukufu kwa vitendo kwa kusaidia jamii ya Zanzibar ili iwe na afya njema iweze kufanya kazi ya kulijenga taifa hili.